

Nakala ya Mazungumzo Wazi kuhusu Chanjo ya Johnson + Johnson

[Muziki mchangamfu]

[Kichwa kwenye Skrini] Mazungumzo Wazi kuhusu chanjo ya Johnson + Johnson

[Dkt. Nathan Chomilo]Hujambo, Mimi ni Dkt. Nathan Chomilo, na niko hapa nikiwa na Adriana Galván. Tuko hapa kuzungumza kuhusu chanjo ya Johnson and Johnson ya COVID-19 na kujibu maswali yoyote tulio nayo kuhusu chanjo za COVID-19 kwa ujumla. Adriana, unaendeleaje?

[Adriana Galván] Ninaendelea vizuri daktari. Asante kwa nafasi hii.

[Chomilo] Kweli, asante kwa mazungumzo haya. Kwa hivyo, je, una maswali yoyote kuhusu chanjo ya Johnson and Johnson?

[Galván] Kweli, naam, la kwanza ni, mwanzoni wakati chanjo ya Johnson and Johnson ilianza kutolewa, ilisitishwa. Na ningependa kujua kilichotokea.

[Chomilo] Kweli. Kwa hivyo, tunafuatilia kwa karibu kuhusu usalama wa chanjo zote. Na kwa hivyo kile kilichojulikana ni kwamba kulikuwa na watu waliokuwa wakipewa chanjo ya Johnson and Johnson ambao walikuwa wanakabiliwa na kuganda kwa damu. Na kwa hivyo ilisitishwa ili kujua kama hali hii ilihusiana na chanjo, na pia kuhakikisha kuwa madaktari na wauguzi wengine walijua kuhusu shida hii ili iweze kutibiwa. Na kile tulichopata ni kwamba kuna hatari ndogo ya kuganda kwa damu unapopata chanjo ya Johnson and Johnson. Hatari hiyo inaonekana kuwa ni kubwa zaidi ikiwa uko chini ya umri wa miaka 50 na wewe ni mwanamke. Lakini juu ya yote, ni hatari ndogo sana. Na kwa kweli, hatari ya kupata mgando wa damu ni kubwa zaidi, ikiwa una COVID-19 yenyewe. Na kwa hivyo bado tunapendekeza chanjo ya Johnson and Johnson kwao kujilinda dhidi ya COVID-19. Je, umekuwa ukisikia nini kutoka kwa jamii kuhusu chanjo ya Johnson and Johnson?

[Galván] Kweli, kando na wasiwasi, jambo moja ambalo ni muhimu kutaja ni kwamba watu wanaipenda kwa sababu ni dozi moja tu. Wakati unafikiria kuhusu chanjo ni muhimu kila mara kwa kila mtu kujua ikiwa ziko salama. Je, chanjo ziko salama kwa kiasi gani kwa sasa?

[Chomilo] Tunajua kwamba chanjo hizi zote ni salama sana, zina ufanisi mkubwa. Na zinasaidia kutulinda sisi na jamii yetu kutokana na COVID-19. Na kwa hivyo hatuna mapendekezo maalum kuhusu ile ambayo utapewa, kwa hivyo fanya utafiti wako, uliza maswali yako na kisha upange kupata moja. Yoyote unayohisi ni salama kwako, ndio tunapendekeza. Na jamii zetu zote zinaweza kupata chanjo zote tatu, na ninadhani ni jambo nzuri sana. Na, na tunataka tu kuhakikisha kuwa watu wanajua hilo. Mimi mwenyewe nimepata chanjo yangu ya COVID-19. Umepata yako?

[Galván] Ndiyo, Nilipata. Nilihisi vizuri. Ninadhani ni salama zaidi. Ninaweza kuwa karibu na marafiki na wapendwa wetu.

[Chomilo] Kweli. Kweli. Na kupata, kupata chanjo dhidi ya COVID-19, bila kujali ni chanjo gani ndilo lengo kwa sababu inatuwezesha kurudi katika hali ya kawaida. Kurudi kwenye zile nyakati ambazo tunazikosa sana. Kuweza kutumia wakati katika kusherehekea, kuwa karibu na wapendwa, kuwa katika jamii. Na kwa hivyo ninatumahi jamii zetu zitapata chanjo na kutupea hiyo kinga ya jamii.

[Galván] Kwa hivyo tunaweza kuhitimisha kuwa, bila kujali chanjo, jambo muhimu hapa ni kwa watu kupata chanjo.

MAZUNGUMZO WAZI KUHUSU CHANJO YA JOHNSON +JOHNSON

[Chomilo] Kabisa, kabisa. Fanya kile unachohitaji kufanya ili kupata habari ili uweze kuhisi vizuri. Kwamba unaweza kufanya uamuzi salama na mpango wa kujikinga wewe pamoja na familia yako. Lakini mwishowe kabisa ili tuweze kutoka kwenye janga hili, tunahitaji kupata chanjo. Kweli, asante sana kwa mazungumzo haya. Yamekuwa ya kufana sana.

[Galván] Asante daktari.

[Muziki mchangamfu]

[ujumbe kwenye skrini] Kwa maelezo zaidi, tembelea:

CDC: Chanjo Yako ya COVID-19 www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/your-vaccination.html

MDH: Kuhusu Chanjo ya COVID-19 www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/vaccine/basics.html

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

6/24/21 (Swahili)

Ili kupata maelezo haya katika muundo tofauti, piga simu kwa: 651-201-4989